


# MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

An abstract graphic design in green ink on a light brown, textured paper background. The design consists of numerous sharp, angular shapes, some solid green and others outlined, radiating from the bottom left corner towards the top right. These shapes vary in size and orientation, creating a sense of dynamic movement and depth. The overall effect is reminiscent of a stylized sunburst or a fan of rays.

Umoja wa Wanawake  
Waenezao Injili

**MIPANGO YA  
USHIRIKA  
MPYA**

*(Part 2 of 2)*

**Umoja wa Wanawake  
Waenezao Injili**

Copyright, 1985  
Baptist Publications House  
All rights reserved

Second Edition 1985

~~First Edition 1985~~

Published and Printed by  
**BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE**  
Thika Road, Ruaraka  
BOX 30370, NAIROBI

*Kenya  
Baptist  
Union*

## YALIYOMO

### MPANGO

### UKURASA

|                                                 |    |
|-------------------------------------------------|----|
| 1. Kwa Nini Twahitaji Kuokolewa? .....          | 5  |
| 2. Nifanye Nini ili Niokolewe? .....            | 8  |
| 3. Biblia .....                                 | 11 |
| 4. Kanisa .....                                 | 14 |
| 5. Amri za Ubatizo na Chakula cha Bwana .....   | 17 |
| 6. Serikali na Madaraka ya Kanisa .....         | 19 |
| 7. Habari za Kueneza Injili Katika Biblia ..... | 22 |
| 8. Jinsi ya Kushuhudia .....                    | 26 |
| 9. Yeye Aiponyaye Roho ni Mwenye Busara .....   | 29 |
| 10. Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili .....  | 33 |
| 11. Shabaha Zetu .....                          | 37 |
| 12. Viongozi na Washiriki na Kazi Yao .....     | 41 |
| 13. Wanawake Wabatisti Wajiunga Pamoja .....    | 44 |

## UMOJA WA WANAWAKE

### WAENEZAO INJILI

Makanisa ya Wabatisti

Rafiki Yetu Mpendwa,

Kitabu hicho kimeandikwa kukusaidia unapofikiri juu ya Ukristo na Kanisa la Kibatisti. Tunatumaini kitakusaidia kukata shauri kumkiri Yesu kama Mwokozi wako. Baada ya kumkiri Yesu, unakaribishwa kujiunga na Kanisa la Kibatisti na kufanya kazi pamoja na wanawake wengine Wabatisti.

Ukisoma mpango mmoja kila wiki, utamaliza kitabu baada ya muda wa miezi mitatu. Ukiwa na maswali, kiongozi wa wanawake au mchungaji wa Kibatisti atafurahi kuyajibu maswali yako.

Asante sana,

Waandishi wa Kitabu,  
Kamati ya Wanawake,  
Misheni ya Kibatisti,  
Afrika ya Mashariki.

## **MPANGO WA KWANZA**

### **KWA NINI TWAHITAJI KUOKOLEWA?**

**Wimbo**  
**Maombi**  
**Wimbo**

**UTANGULIZI:** (Kiongozi) 'Hapo mwanzo Mungu...' haya ndiyo maneno ya kwanza katika Biblia, ambayo ndiyo Neno Takatifu la Mungu.

Tuanzapo masomo pamoja katika Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili twahitaji kujiuliza swali hili: 'Kwa nini twahitaji kuokolewa?' Katika Yohana 3:16 twasoma, 'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.' Bila kumwamini Yesu, Mwana wa Mungu, hatuwezi kupata uzima wa milele. Tukimkubali Yesu kama Mwokozi, Mungu atatupa sisi kipawa kile cha wokovu. Na ebuni tuangalie katika Biblia zetu ili tulifahamu jambo hili vema.

**SEHEMU YA KWANZA:** Mungu Ndiye Mwumbaji wa Vyote

Mungu alikuwako, hata kabla ya dunia kuumbwa. Aliumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo. Kiumbe chake kikuu hasa kilikuwa mwanadamu, ambaye alimwumba katika sura yake mwenyewe. Mungu alimpenda binadamu na hata akampa uwezo juu ya viumbe vyote. Naye alishirikiana na Mungu kila siku.

**SEHEMU YA PILI:** Mwanadamu Akatenda Dhambi

Mungu alikuwa amewapa mtu na mkewe mahali pazuri sana kuishi. Lakini Ibilisi, adui wake Mungu, aliwajaribu siku moja nao wakakosa kumtii Mungu. Hii ndiyo dhambi yao ya kwanza nao ushirika waliokuwa nao na Mungu ukavunjwa. Ikawabidi kuacha

nyumba yao nzuri na ikawapasa kufanya kazi ili wapate kuishi. Na baada ya hiyo, mwanadamu akaendelea kutoa dhabihu kwake Mungu ili aweze kusamehewa dhambi alizozifanya na pia waweza kushirikiana pamoja na Mungu.

**SEHEMU YA TATU: Mungu Alituma Mwanawe**

Miaka mingi ilipita nao watu walikuwa wameongezeka duniani. Watu wengi walikuwa wamemsahau Mungu nao walikuwa waovu sana. Ni watu wachache tu ambao walimpenda hata wakamtumikia. Mwishowe Mungu alitambua ya kwamba ni lazima amtume Mwanawe, Yesu Kristo, aishi duniani na kufa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Kwa hiyo Yesu Mwana wa Mungu aliyekuwa mwema, kamili kabisa, alizaliwa kama mwanadamu akaishi kwa muda wa miaka thelathini na mitatu duniani. Lakini hata hivyo watu hawakumgeukia Mungu. Yesu aliwaelezea habari za Baba yake aliyekuwa mbinguni, yaani Mungu, lakini ni kundi dogo tu lililomfuata. Na mwishowe alisulibiwa msalabani hata akafa.

**SEHEMU YA NNE: Yesu Anao Uwezo Juu ya Kifo**

Yesu alipokufa msalabani, alisulibiwa kwa ajili ya watu wote, hata kwa ajili yako nami. Baada ya siku tatu alifufuka kutoka kaburi lake. Alikuwa mshindi juu ya kifo. Naye ataishi kwa milele. Kwa kweli alikuwa Mwokozi. Yesu alirudi mbinguni kuwa pamoja na baba yake tena, lakini akawaambia watu wake, 'Mnamwamini Mungu, mnamwamini hata mimi' (Yohana 14:1). Ukimwamini Yesu Kristo hata ukamfuata yeye, utapata maisha ya milele nazo dhambi zako zitasamehewa. Yesu alisema, 'Hakuna mtu ye yote ajaye kwa Baba isipokuwa kwa njia nami' (Yohana 14:6).

**KIONGOZI:** Sisi twaweza kumshukuru Mungu kwa kuwa alitupenda sisi hata akamtoa Mwanawe ili afe kwa ajili ya dhambi zetu. Nami nafikiri ya kuwa kwa sasa twaweza kulijibu swali hili, 'Kwa nini twahitaji kuokolewa?' Ebu, na tuombe ya kwamba sisi wenyewe tuweze kujua ya kwamba wokovu ndio mlango wa kuingia

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

maisha ya milele na ya kuwa tutaweza kuamini katika Yesu Kristo,  
Mwana wa Mungu.

## **MPANGO WA PILI**

### **NIFANYE NINI ILI NIOKOLEWE?**

**Wimbo**  
**Maombi**

**UTANGULIZI:** (Kiongozi) Tulizungumza wiki iliyopita juu ya 'Kwa nini twahitaji kuokolewa?' Na sasa, ni lazima tujiulize swali hili: 'Nitaifanya nini ili nipate kuokolewa?' Katika kitabu cha Yohana twasoma habari za mtu mmoja aliyemjia Yesu akamwuliza swali hili. Ebu niwasomee jibu lake Yesu. (Soma Yohana 3:5 na 16-17.) Yesu alimwambia huyo mtawala wa Wayahudi ya kwamba ni lazima azaliwe tena. Kwa mara ya kwanza twazaliwa kwa mwili kama watoto wachanga. Na pia yatupasa tuzaliwe kwa roho. Nayo hii yawezekana tu tukimwamini Yesu.

**SEHEMU YA KWANZA:** Binadamu Huzaliwa Katika Dhambi

(Soma Warumi 5:12). Ikiwa tutamwamini Yesu, kwanza ni lazima tujue ya kuwa sisi sote ni watenda dhambi. Baada ya kufahamu ya kuwa sisi tu watenda dhambi kila siku, ni lazima tumwombe Mungu atusamehe dhambi zetu. Mungu aweza kusafisha dhambi zetu zote kutoka maisha yetu naye aweza kutufanya kuwa wema. Warumi 6:23 husema, 'Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo bwana wetu.' Na mpaka tumemwomba Mungu kuondoa dhambi zetu na pia kumwomba atusamehe, hatuwezi kuwa na uzima wa milele.

**SEHEMU YA PILI:** Kuwa na Imani Katika Kristo Huleta Uzima wa Milele

(Soma Matendo 16:30-31). Na kwa sababu twajua sasa ya kuwa sisi huzaliwa katika dhambi nasi twashinda katika dhambi, yatupasa

tumwamini Bwana Yesu Kristo nasi tutaokolewa. Yatupasa kuweka imani yetu na uaminifu wetu katika Mwana wa Mungu, kuamini ya kuwa yeye ndiye aliye kweli na mkamilifu. Anaweza kusafisha mioyo yetu kutoka dhambi na kutupa sisi maisha ya milele. Na dakika ile utakaposema "Naamini" moyoni mwako, Yesu ataingia na ataishi pamoja nawe kwa milele

### **SEHEMU YA TATU: Mkristo ni Kiumbe Kipya**

(Soma 2 Wakorintho 5:17). Na mara tu tunapomkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wetu, sisi huwa viumbe vipya. Kristo huwa ameingia mioyoni mwetu na kuishi ndani yetu. Yeye huleta amani na furaha. Nasi huwa na ushirika mmoja na Mungu katika Mwanawe, Yesu. Nasi twaweza kumwomba atusaidie kila siku na kumfuata na kumtumikia. Hili ni jambo rahisi, lakini twajua ya kuwa anaweza kutupatia msaada. Kristo ametuambia ya kwamba sisi ndio watoto wa Mungu, naye ndiye Baba yetu.

### **SEHEMU YA NNE: Ni Lazima Mkristo Amfuate Yesu**

(Soma Mathayo 16:24-27). Sisi tukiwa Wakristo ni lazima tumfuate Yesu kila siku. Tumtumikie Yesu bila kujifikiria kwa kumweka Yesu kwanza katika maisha yetu. Tunapomfuata Yesu, yeye atatuongoza siku zote. Kwa kusoma na kujifunza Neno la Mungu twaweza kujifunza vile tuwezavyo kumtumikia Kristo na namna ya kuwaambia watu wengine habari zake. Alisema, 'Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu.' (Yohana 12:26)

**KIONGOZI:** Tufanye nini ili tuokolewe? Ni lazima kwanza kujua ya kuwa tu watenda dhambi. Halafu ni lazima tuombe Mungu ili atusamehe dhambi zetu na kumruhusu Kristo aingie katika mioyo yetu na katika maisha yetu. Tumwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, naye atatupatia maisha ya milele. Tunapomwamini Yesu, ni lazima tumfuate. Na sasa tuinamishe vichwa vyetu kwa kuomba.

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

(Wakati huu ni muhimu sana kwa wanawake wa kundi lako. Waongoze katika maombi na kuuliza wale ambao si Wakristo kumfuata Kristo kama Mwokozi wao. Waongoze wale ambao ni Wakristo kuomba Mungu kuwasaidia katika kumfuata na kumtumikia. Wape wanawake nafasi ya kusema, 'Naamini.')

## **MPANGO WA TATU**

### **BIBLIA**

**Wimbo**

**Maombi**

**Maandiko:** 2 Timotheo 3:16-17

**Wimbo**

Biblia ni Neno la Mungu. Mungu hujifunua kwa watu wanaoisoma Biblia na kutafuta maana yake. Sisi tukiwa Wabatisti tumeamini mambo kadha juu ya Biblia na maana yake.

#### **SEHEMU YA KWANZA:**

Kwanza, tunaamini ya kuwa wale walioandika Biblia waliongozwa na Roho Mtakatifu. Katika 2 Petro 1:21 tunasoma, 'Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.'

Tunaamini ya kwamba tunapaswa kutafuta vile maandiko yanavyonena kuhusu jambo fulani halafu kufuata mafundisho yake. Ni lazima Biblia iwe na mamlaka kamili na mwisho Biblia iwe kiongozi chetu katika mambo yote ya dini. Tunaamini ya kwamba Biblia imefunua yote ambayo ni sharti kujua ili tuweze kufahamu na kukubali kipawa cha wokovu wa Mungu. Kwa kuisoma Biblia mtu ataweza kuifahamu hali yake ya upotevu na itamwongoza kutubu na kumwamini Mungu. Soma Waebrania 4:12.

Pia tunaamini ya kuwa Biblia haiwezi kuangamizwa, na kwamba ni ya milele na ya kudumu. Soma Mathayo 24:35.

#### **SEHEMU YA PILI:**

Biblia imegawanyika kwenye makundi mawili, Agano la Kale na Agano Jipya, na makundi hayo yamegawanyika kwenye vitabu

## **MIPANGO YA USHIRIKA MPYA**

mbalimbali. Agano la Kale ni hadithi za watu wa Mungu kabla ya kuzaliwa kwake Kristo. Agano Jipya ni hadithi ya kuzaliwa kwake, pamoja na kazi yake na mafundisho ya wafuasi wake.

Kuna vitabu 39 katika Agano la Kale na vitabu 27 katika Agano Jipya, vyote pamoja ni vitabu 66. Vitabu hivi viliandikwa kwa nyakati mbalimbali na watu mbalimbali. Baadhi yao walikuwa wachungaji na wakulima, wengine walikuwa wafalme, wavuvi, waalimu na wafanyi biashara. Wengi wa waandishi hao hawakuwajua waandishi wengine, hata hawakuandika katika njia moja, lakini kila mmoja anaeleza ujumbe wa pendo la Mungu kwa watu wote.

### **SEHEMU YA TATU:**

Agano la Kale liliandikwa katika lugha ya Kiebrania, ambayo ni lugha ya Waisraeli. Maandishi yamegawanyika kwa njia hii, tukianzia katika mwanzo wa Biblia. Vitabu vitano vya kwanza ni vitabu vya torati vilivyoandikwa na Musa; vitabu vingine kumi na viwili ni historia ya watu wa Waebrania; vitabu vingine vitano ni vitabu vya mashairi vilivyoandikwa na Daudi na wale wengine; vitabu vingine vitano ni unabii mrefu na vitabu kumi na viwili ni unabii mfupi. Manabii walieleza habari za kuja kwake Mwokozi katika siku ya usoni. Watu wengi waliliamini jambo hili na walikuwa wakitazamia kuja kwake.

### **SEHEMU YA NNE:**

Agano Jipya liliandikwa kwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiyunani kwa sababu lugha hiyo ilikuwa ikitumiwa katika nchi nyingi wakati wa Yesu. Vitabu vinne vya kwanza ni vitabu vya Injili vilivyoandikwa na Mathayo, Marko, Luka na Yohana. Kitabu cha Matendo ya Mitume ni historia au matendo kama walivyoongozwa na Roho Mtakatifu.

Paulo aliandika vitabu vingine 13 vinavyofuata, ambavyo ni nyaraka alizowaandikia marafiki zake au makanisa kuwasaidia

kukua katika maisha yao ya kiroho. Kuna vitabu vingine vinane katika Agano Jipya, vilivyoandikwa na watu wengine. Hizo ni nyaraka fupi lakini zina mafundisho makuu ambayo yatatusaidia katika maisha yetu ya Kikristo.

Kitabu cha mwisho katika Biblia yetu ni Ufunuo wa Yohana, ambacho ni kitabu cha unabii na hueleza habari za kurudi kwake Yesu ulimwenguni kwa kuwakusanya wafuasi wake pamoja.

Biblia ni kitabu cha maana zaidi kuliko vitabu vingine vyote na sisi Wakristo tunapaswa kukisoma kila siku, na kufuata mafundisho yake, na kutafuta kuwaongoza watu wengine kwenda kwake Mungu.

## **MPANGO WA NNE**

### **KANISA**

**Wimbo**

**Maombi**

**Maandiko:** Mathayo 16:15-18

**Wimbo**

Mara kwa mara tunafikiri kanisa ni jengo ambapo tunakutanika kuabudu, au ni nyumba ya Mungu, au nyumba ya kusali. Lakini maana halisi ya neno 'Kanisa' ni zaidi ya hayo. Kwa kuisoma Biblia tunaamini ya kuwa Kanisa ni kundi la wenye kuamini na kubatizwa katika Kristo, ambao wanakubali kujiunga pamoja kwa ajili ya ibada na kuendeleza kazi ya Kristo.

#### **SEHEMU YA KWANZA:**

Yesu alisema ya kuwa analijenga kanisa lake juu ya imani, imani kama ile ya wanafunzi Wake walioamini kuwa Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu aishiye. Paulo ameandika mengi kuhusu kanisa. Amesema ya kuwa Kristo ndiye kichwa cha Kanisa na kazi yake yote inahitaji kufanywa kwa uongozi wake. Yeye ndiye katikati na kifungo cha umoja wa vitu vyote. Kwa sababu yeye ni Bwana wa maisha ya Mkristo, anapaswa pia kutawala kama Bwana katika ushirika wa Wakristo katika Kanisa fulani. Ni wajibu wa kila kanisa kumwinua Kristo kuwa kama Kichwa.

#### **SEHEMU YA PILI:**

Katika 1 Wakorintho 12 Paulo anaeleza kanisa kama mwili wa Kristo. Halafu analifananisha kanisa na mwili wa mwanadamu. 'Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, na mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo' (1 Wakorintho 12:12). Washiriki wote wa mwili ni lazima wafanye kazi pamoja - mguu, sikio, jicho, mkono, ili ndipo mwili

uweze kutenda kazi yake kwa njia ya kufaa. Kama viungo hivi visipofanya kazi pamoja na katika umoja basi mwili wote huugua. Kila kiungo cha mwili wa mwanadamu hutegemea kile kiungo kingine cha mwili. Vivyo hivyo ndivyo kweli kwa washiriki wa mwili wa kanisa.

### SEHEMU YA TATU:

Kanisa huundwa na wenye kumwamini Kristo. Ni wale tu ambao wamemkiri Kristo kwa njia ya imani ambao wataweza kukubaliwa kuingia na kuwa washiriki wa kanisa. Baada ya kukiri kwake Petro ndipo Yesu aliposema, 'Nitalijenga kanisa langu' (Mathayo 16:18). Tena Yesu alisema ya kuwa 'mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.' Mafundisho yaliyoko ndani ya kifungu ni kwamba kanisa la Kristo litaweza kuanzishwa ndani ya mioyo ya wenye kuamini ambao wameangaziwa na Roho wa Mungu na kumkiri Kristo mbele za ulimwengu.

### SEHEMU YA NNE:

Ikiwa sisi tu kanisa basi ni lazima tuendeshe shughuli zake katika hali ya Kikristo. Kanisa linajitawala. Washiriki wake wote wanayo haki sawa katika kuzungumza na kupiga kura katika shughuli zake. Kila kanisa ni lazima liwe na mikutano kwa kawaida ambapo viongozi hutoa taarifa ya kazi yao na washiriki huzungumza katika kuendesha kazi za kanisa. Wafanye hivi pia kuhusu sadaka na matumizi yanayotukia katika kuendesha kazi za kanisa.

Agano Jipya limetaja 'kanisa' mara 85 kueleza habari za kundi la Wakristo la mahali fulani. Haiwezekani kujaribu kuliweka kanisa moja la ulimwengu wote ili watu wote wawe ndani yake. Wanaume na Wanawake wote waliokombolewa wa kila umri ni wa ukoo wa jamii ya Mungu. (Waefeso 3:15). Kila mwamini aliyezaliwa upya huwa yumo ndani ya Ufalme wa Mungu. (Yohana 3:15). Lakini ni

## **MIPANGO YA USHIRIKA MPYA**

**watu waliobatizwa tu ndani ya kanisa la mahali fulani, ambao hutumia Agano Jipya kama amri yao. Wao ndio Kanisa la Agano Jipya.**

## MPANGO WA TANO

### AMRI ZA UBATIZO NA CHAKULA CHA BWANA

**Wimbo**

**Maandiko:** Warumi 6:1-4

**Maombi**

**Wimbo**

Makanisa yetu hutii amri mbili - amri ya ubatizo na Chakula cha Bwana. Huitwa amri kwa sababu ziliamriwa na Kristo ili kanisa liwe likizitii.

#### SEHEMU YA KWANZA:

Makanisa ya madhehebu mengi hubatiza katika njia mbalimbali. Wabatisti wanaamini ya kuwa Biblia imefundisha ya kuwa ni lazima mtu kubatizwa kwa kuzamishwa majini. Soma Mathayo 3:16. Maandiko yanasema ya kuwa Yesu alipobatizwa alitoka majini. Yesu alibatizwa kwa kuwaonyesha wanafunzi wake ya kuwa wanapaswa kushuhudia imani yao kwa kumfuata yeye katika ubatizo.

#### SEHEMU YA PILI:

Ubatizo ni picha ya kuonyesha vile Kristo alifanya kwa ajili yetu. Alikufa, akazikwa, na kufufuka tena ili tupate kuwa na maisha mapya ndani yake. Katika ubatizo, tunapoingia majini ni picha kufa katika maisha ya kale na kuzaliwa upya katika Kristo. Mtu anapookolewa huwa anaweka mbali maisha yake ya kale yenye dhambi na sasa anakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu.

#### SEHEMU YA TATU:

Ni wale tu ambao wamekiri imani yao katika Kristo ndio wapasao kubatizwa. Hakuna uwezo wa kuokoa katika kitendo cha ubatizo. Katika Mathayo 3 wakati Mafarisayo na Masadukayo

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

walipomwendea Yohana kubatizwa, aliwakemea na kuwaambia wazae matunda na kutenda mambo ambayo yanaonyesha ya kuwa wamebadilika kutoka dhambini. Ni baada ya kutubu na kuwa na imani ambapo ubatizo huwa na maana kwa mtu ye yote. Kwa hiyo sisi Wabatisti hatuwabatizi watoto wachanga. Kama mtoto akifundishwa Neno la Mungu na kufikia kwenye ufahamu wa uwezo wa Mungu wa kuokoa, basi ataweza kumkubali Kristo kama Mwokozi, na baadaye abatizwe.

## SEHEMU YA NNE:

Soma Matendo 2:41-42; na 1 Wakorintho 11:26. Tunaadhimisha Chakula cha Bwana kwa kukikumbuka kifo cha Bwana wetu - kuvunjwa kwa mwili wake na damu yake iliyomwagika.

Yesu aliumega mkate na kukinywea kikombe pamoja na wanafunzi wake. Aliwapa mkate, kuwa ishara ya mwili wake na kikombe kikisimamia damu yake. Na walipoimba wimbo walitoka nje na kwenda kwenye mlima wa mizeituni.

Tumeambiwa kuumega mkate na kukinywea kikombe kumkumbuka yeye. Je! ni nani mwenye haki yakuadhimisha Chakula cha Bwana? Ni amri ya kanisa kwa ajili ya wale ambao wamemwamini na wale wanaotafuta kuyafuata mafundisho yake na kuyatenda mapenzi yake. Ubatizo hauna maana kwa mtu ambaye hajaokolewa. Tumeambiwa kufanya hivyo kumkumbuka yeye, lakini hakutuambia ni mara ngapi tuwezavyo kufanya jambo hilo. Kila kanisa lina uhuru wa kuchagua wataadhimisha lini na mara ngapi.

Kuadhimisha Meza ya Bwana ni kuyasitawisha maisha ya kiroho na kunapaswa kufanywa na kila aminiye katika ushirika wa kanisa.

## **MPANGO WA SITA**

### **SERIKALI NA MADARAKA YA KANISA**

**Wimbo**

**Maandiko:** Wakolosai 1:15-20

**Maombi**

**Wimbo**

Je! ni kwa njia gani makanisa yenu yalipata kuwa jinsi yalivyo?  
Je! kwa nini yalitungwa kwa njia hii? Ebu na tutazame katika Agano  
Jipya na kuona vile kanisa la kwanza la Kikristo lilivyoanza.

#### **SEHEMU YA KWANZA:**

Hakuna habari zilizoandikwa juu ya kanisa lililotungwa wakati wa maisha ya kuhubiri kwake Kristo ulimwenguni. Aliliandaa kanisa ndani ya maisha ya wanafunzi wake na kuwapa maagizo na amri kuu. Aina ya kutungwa kwa kanisa kulitokea kwa njia ya kukua na kama vile haja zilitukia. Yudasi alikuwa mweka hazina, mashemasi walichaguliwa wakati ulipotimia. Wakati huo kanisa lilikuwa limengojea na kuomba kwa muda wa siku kumi kabla ya siku ya Pentekoste. Kutoka katika kanisa la kwanza wanafunzi walitoka nje kwenda kuyaanzisha makanisa mengine kwa njia ya kusudi lililo sasa. Ni haki tufuate mafundisho yote ya Agano Jipya.

#### **SEHEMU YA PILI:**

Wakati wa Pentekoste Petro alieleza masharti ya kukubaliwa kuingia katika ushirika wa wanafunzi Wakristo; toba, imani na ubatizo, Matendo 2:41. Msingi wa kuwa mshiriki wa kanisa umejengwa juu ya kumtubia Mungu na kuwa na imani katika Bwana Yesu Kristo, na halafu kufuatiwa na ubatizo.

Ni wazi katika Agano Jipya kwamba makanisa ya hapo mwanzo yalifahamu na kutekeleza serikali hii ya kidemokrasi. Mtu wa kuitenda kazi ya Yudasi alichaguliwa na washiriki wote 120 wa

## **MIPANGO YA USHIRIKA MPYA**

kanisa la Yerusalemu. Baadaye wasaidizi wengine saba walichaguliwa na kanisa. Kanisa lililokuwa katika Antiokia, likifanya kazi kama kundi, baada ya kufunga kula na kuomba, waliwawekea mikono Baranaba na Paulo wakawatuma kwenda katika safari yao ya kwanza ya umisheni.

## **SEHEMU YA TATU:**

Makanisa yetu katika eneo fulani huweza kujiunga pamoja na kuwa na Jumuiya Ndogo ya eneo na halafu kujiunga na Jumuiya Kuu, lakini shirika hizi hazina mamlaka juu ya kanisa la mahali pengine.

Uhusiano wa kanisa na serikali ya utawala uwe jambo moja lililo tofauti na lingine, lakini kila moja huheshimu ile nyingine. Kila nchi inapaswa kutoa uhuru kwa raia wake kuabudu jinsi wapendavyo. Pia kanisa halipaswi kutafuta kuwa na mamlaka juu ya serikali ya taifa.

## **SEHEMU YA NNE:**

Ni wajibu wa kila kanisa kufundisha washiriki wake kulifahamu Neno la Mungu, na jinsi kila mshiriki anaweza kuieneza injili kwa watu wengine. Katika makanisa ya Kibatisti jambo hili kufanywa kwa njia ya Shule ya Jumapili kwa kuwa wanaume na wanawake kufundishwa, na hata watoto pia. Jamii yote itaweza kushiriki katika hili kanisa.

Wanawake na watoto hukutanika katika shirika zao zilizo mbalimbali wakati wa juma ili wajifunze na kuomba, na kushirikiana. Kusudi lake ni kukua katika mambo ya kiroho, kuhusika na haja za watu wengine, na kutafuta njia za kuwasaidia watu hao. Shirika la wanawake huitwa "Umoja wa Wanawake Waenezao Injili." Kundi la wasichana na wavulana huitwa 'Wajumbe wa Yesu.'

Ibada Kuu ya maombi siyo shirika lakini ni sehemu ya kawaida iliyo ya maana. Wakati huu tunapaswa kusikiliza Neno la Mungu na kufikiria maana yake katika maisha yetu. Ni wakati wa kusikiliza vile Mungu anavyosema kwa mioyo yetu. Kuhudhuria ibada hii ni ushuhuda kwa watu wengine juu ya imani yetu kwake Mungu.

## **MPANGO WA SABA**

### **HABARI ZA KUENEZA INJILI KATIKA BIBLIA**

#### **Wimbo**

**Maandiko:** 'Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Bana, na Mwana, na roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

Mathayo 28:19-20

#### **Maombi Wimbo**

#### **KIONGOZI WA MPANGO:**

Katika somo hili tutajifunza juu ya kazi ya kueneza injili katika Biblia. (Inua Biblia juu.) Biblia ni kitabu kinachoeleza juu ya kutangaza ujumbe wa Mungu, yaani, kushuhudia watu wote katika sehemu zote. Na katika Biblia nzima twapata ujumbe huu. Mungu awapenda watu wote. Naye hutaka watu wote kuokolewa. Naye ahitaji watu wake wote wawe wajumbe wake ili wamshuhudie yeye.

#### **SEHEMU YA KWANZA: Katika Zaburi**

Waandishi wa Zaburi wanasema juu ya siku ile ambapo mataifa yote yatapata habari ya Bwana na wokovu wake. Vifungu hivi vyote viliimbwa na wateule wa Mungu katika hekalu. Mara nyingi waliimba nyimbo hizi ambazo zasema kwamba Mungu anataka watu wote kuokolewa kwa namna yake ya ukombozi.

(Soma Zaburi 67.) Zaburi hii yaanza kwa maombi kwamba Mungu aweza kuwabariki watu wake wateule ili njia yake iweze kujulikana ulimwenguni mwote. Na wokovu wake ujulikane katika mataifa yote. Nao watu wanatakiwa kumtukuza Mungu na kuabudu mbele za hakimumu wa mataifa yote. Nayo Zaburi hii yamaliza kwa

kueleza kwamba kusudi la Mungu duniani kote litatimizwa. Mungu atatubariki sisi na nchi yote itamwogopa na kumtumikia yeye.

**SEHEMU YA PILI: Katika Agano la Kale**

Naamani alikuwa akipiga vita na Waisraeli, wateule wa Mungu. Nao wakamshika msichana mdogo. Akawa mtumishi wa mkewe Naamani. Na mara tu akatambua kwamba Naamani alikuwa na ugonjwa wa ukoma. Na mara tu huyo msichana mdogo akamkumbuka Elisha aliyeshi nyumbani. Alikumbuka vile alivyokuwa amewasaidia watu wengi. Naye huyo msichana mdogo akaanza kumwelezea mke wa Naamani juu ya mtu huyo wa Mungu. Akamwambia mambo yote ambayo Elisha alimfundisha. Naye alikuwa akishuhudia kwa ajili yake Mungu katika nchi hiyo geni. Akamwambia mkewe Naamani kwamba Mungu wa Elisha anaweza hata kuponya ugonjwa huu wa ukoma. Na baada ya Naamani kuponywa ugonjwa wake wa ukoma alimsifu Mungu wa Elisha. Na kwa sababu ya msichana huyo mdogo, Naamani alijifunza habari za Mungu wa kweli. Kwa kweli alikuwa mmisheni kamili hata ingawa alikuwa mtumishi.

Sisi sote tunaweza kueneza injili kama msichana mdogo alivyofanya. Je! uko tayari kuyafanya mambo yaliyo ya haki hata ingawa wengine wanafanya yasiyo ya haki? Ikiwa twampenda Mungu tutamshuhudia. Sisi tutawaleta watu wengi kwake Mungu tukiishi kwa ajili yake kila siku.

**SEHEMU YA TATU: Katika Agano Jipya**

Katika Agano Jipya Yesu anatuonyesha wazi ya kwamba alitumwa na Mungu ili afundishe ujumbe wa pendo lake Mungu na wokovu kwa mataifa yote. Alifundisha ya kwamba ufalme wa mbinguni umefunguliwa kwa watu wote wa makabila yote na hali zote siyo kwa Wayahudi peke yao. Nao wote wawe kabila moja katika Yesu Kristo. Yesu aliwakaripia Wayahudi, watu wake wenyewe, kwa kuwa hawakuwapenda watu wa mataifa mengine.

## **MIPANGO YA USHIRIKA MPYA**

Yesu aliwaambia viongozi wa Wayahudi hadithi ya Msamaria mwema ili awaonyeshe vile walivyoonyesha ubaguzi. (Soma Luka 10:25-31 na usimulie hadithi hiyo). Katika hadithi hii Yesu alionyesha wazi vile Wayahudi walivyokuwa na ubaguzi na vile walivyojifikiria wao tu kwa sababu waliwachukia watu wa makabila mengine ambayo hawakuwa Wayahudi.

### **SEHEMU YA NNE: Mfano wa Kristo**

Kristo aliamuru Wakristo wote kueneza habari za injili kila mahali. Sisi tumeambiwa tuwafanye watu wote kuwa wafuasi wake. Huu sio mwaliko. Ni amri. Bwana hatarajii ya kwamba baadhi ya wafuasi wake tu ndio watakaoshuhudia bali huwaambia wote washuhudie. Ikiwa Kristo ni Bwana na Mtawala wetu basi sisi tu watumishi wake. Hatutakuwa tunamtii Bwana ikiwa hatutashuhudia wokovu wake kwa neema zake. Ikiwa sisi tunampenda tutashika amri zake. Watu wote ni chini ya laana ya dhambi naye Kristo haachi mtu ye yote nje ya pendo lake. Hakuna mahali ko kote mmoja aweza kupata msamaha au kusamehewa dhambi zake isipokuwa katika Kristo. Huu ndio ujumbe ambao Kristo aliwapatia wafuasi wake ili wautangazie mataifa yote. Naye pia aliahidi kuwa pamoja nasi tunapoendelea kufanya hivyo.

### **KIONGOZI WA MPANGO:**

Ikiwa kwa kweli tutampenda Kristo, tutashika amri zake. Katika 1 Wakorintho, mlango wa 13, Paulo anatuambia kwamba upendo ni jambo kubwa kuliko mambo yote. Upendo huwako kwa milele. Upendo hauna hasara yo yote. Upendo haushindwi. Tunapofikiria juu ya upendo wa Kristo kwetu sisi, mioyo yetu hujazwa na mshangao.

Kristo hupima mapenzi yetu kwake kwa njia ile tufanyayo mambo ametuamuru. (Soma Yohana 14:21-24).

Kuna hadithi ya mwanamke mmoja aliyekuwa na watoto watatu. Watoto hawa wote walimwambia mama yao kila siku

kwamba walimpenda, lakini ni mmoja tu wa watoto hao aliyemsaidia mama yao kwa kazi. Kila jioni kila mtoto alisema, 'Nakupenda mama.' Lakini mama yao alijua ni mtoto gani ambaye alimpenda zaidi. Haitoshi kusema kwa mdomo wetu kwamba twampenda Kristo. Ikiwa kwa kweli tunampenda, tutaifanya kazi yake.

**MAOMBI:**

Baba yetu, tupe moyo wenye upendo na huruma kwa hao wote wasiokujua wewe. Tufanye tupate nguvu katika kazi yetu ya kushuhudia. Amina.

# **MPANGO WA NANE**

## **JINSI YA KUSHUHUDIA**

**Wimbo:** Nimekombolewa na Yesu

**Maandiko:** Waefeso 2:8

**Maombi**

### **KIONGOZI:**

Ni nani aliyekuambia habari za Yesu? Mhubiri? Mmisheni? Rafiki? Ni nani uliyemwambia habari za Yesu? Jamaa zake? Rafiki zake? Sisi sote twapenda kutangaza habari njema. Na habari njema kuliko zote ni hiyo: 'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.' Yohana 3:16. Mtu fulani ametuambia habari njema hii. Na twataka kuwaambia wengine.

Ni nani ambao tutawaambia habari njema yetu? Ungewaambia akina nani habari njema yo yote? Ungemwambia kila mmoja ufahamuye na labda wageni pia. Kadhalika tufanye hivyo juu ya habari njema za Yesu.

Tunaweza kuwaambia waume zetu na watoto wetu. Tunaweza kuwaambia baba zetu, kaka na dada zetu, na jamaa zetu wengine. Sisi sote tunao marafiki wasio Wakristo. Tunaweza kuwaambia. Kuna watu waishio karibu na nyumba zetu wasiomjua Kristo. Tunaweza kuwaambia.

**SEHEMU YA KWANZA:** Ushuhuda wa Binafsi

Na tutawaambia nini? Kwanza, tunaweza kuwaambia kuwa sisi tu Wakristo. Kisha tunaweza kuwaambia jinsi tulivyo na furaha kwa kuwa Wakristo. Tunaweza kusema tunafahamu ya kuwa sote tu wenye dhambi. Tulipoelewa ya kuwa tulitenda dhambi, tulimhitaji Mungu kutusamehe na kutuokoa kutoka dhambi zetu. Biblia ilituambia hilo: 'Bali tukienenda nurumi, kama yeye alivyo katika

nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi yote' (1 Yohana 1:7). Tena inasema: 'Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote' (1 Yohana 1:9). Kwa hiyo tulitubu kwa Mungu tukakiri kwamba sisi ni wenye dhambi tukamwomba atusamehe. Na tukaamini ya kuwa Yesu atatuokoa. Na akafanya hivyo. Na Yesu atafanya hivyo. Na Yesu akafanya hivyo kwa kila mmoja. Biblia inasema hivyo.

### **SEHEMU YA PILI: Fundisho la Biblia**

Biblia ni kitabu ambacho hutuambia habari za Mungu na upendo wake, kwa hivyo ni vyema kwetu kujua kwa kadiri tuwezavyo juu ya Biblia. Tunahitaji kuhudhuria Shule ya Jumapili kujifunza Biblia. Tunahitaji kujifunza mistari mingi ya Biblia kwa kadiri tuwezavyo. Tunahitaji kujaribu kusoma Biblia. Kisha tunahitaji kushirikiana na wengine katika fundisho hili.

### **SEHEMU YA TATU: Kwa Kuhudhuria Kanisa**

Baada ya kusema yote tuwezavyo juu ya Yesu, pengine rafiki yetu atakuwa na maswali. Kama hatuwezi kuyajibu, tunaweza kumpeleka kwa mhubiri wetu au mwalimu wetu wa Jumapili au mmisheni. Tunaweza kumkaribisha aende kwenye Shule ya Jumapili na huduma za ibada. Itakuwa bora tukienda pamoja.

### **SEHEMU YA NNE: Kwa Maisha Yetu**

Tunaposema habari za Kristo, yatupasa tuwe waangalifu sana, kuishi kwa mfano wake kwa kadiri tuwezavyo. Rafiki zetu wakiweza kumwona Kristo akiishi ndani yetu, itakuwa rahisi kwao kuamini yale tusemayo juu yake.

### **SEHEMU YA TANO: Kwa Maombi**

Sikuzote tunapojaribu kumshuhudia Yesu, yatupasa kuomba ili Mungu atusaidie kuishi maisha ya haki na ili atupe maneno ya

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

kusema yaliyo sawa. Yatupasa kuomba ili Mungu afungue mioyo ya marafiki zetu ili wamwamini Kristo. Kumbuka, sisi wenyewe hatuwezi kumwokoza mtu ye yote. Ni Mungu tu mwenye uwezo wa kufanya hivyo. Anatutumia sisi kama wasaidizi wake tukimkubalia.

Je! Utamwambia mtu habari za Yesu leo?

### MAOMBI

**KIPINDI CHA KUJIFUNZA:** Kila mwanamke ajaribu kujifunza vifungu hivi.

Warumi 3:23: Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

Yohana 3:16: Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Matendo 16:31: Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.

Waefeso 2:8: Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu.

**KUPANGA MBELE:** Wiki ijayo kutakuwa na mchezo wa kuiga. Fanya matayarisho sasa.

## MPANGO WA TISA

### YEYE AIPONYAYE ROHO NI MWENYE BUSARA

**Wimbo:** Waponyeni Watu

**Maombi**

**MAARIFA:** Kila mwanamke apewe nafasi ya kueleza juu ya kazi yake ikiwa amejaribu kushuhudia tangu mkutano uliopita.

#### **KIONGOZI:**

Eleza ya kwamba kazi ya kila Mkristo ni kuvuta watu wengine kwa Kristo. Kusudi la mchezo huu ni kuwasaidia wanawake ili waweze kuwaleta wengine kwa Kristo. Kila mwanamke anapokwenda nyumbani leo aende na kitabu chake ili aweze kuvitumia vifungu vifuatavyo kwa kushuhudia. Wanawake waliohudhuria mkutano wa mwisho wamejifunza baadhi ya vifungu hivi. Wasaidie wanawake kurudia vifungu hivi na kujifunza vile viwili vingine.

Tengeneza orodha ya maombi ya wanawake katika jamii yenu ambao hawajamkiri Yesu. Wanawake wanaohudhuria wanaweza kusaidia kutengeneza orodha hii.

#### **MAANDIKO YA KUJIFUNZA NA KUTUMIA WAKATI WA KUSHUHUDIA:**

**Wote Wamefanya Dhambi:** Warumi 3:23. Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

**Mungu Hutoa Wokovu:** Yohana 3:16. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Waefeso 2:8,9: Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.

**Sisi Huchagua:** Warumi 10:10 Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.

**Hakikisho la Wokovu:** Yohana 5:24. Amin, Amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.

**MCHEZO: Yeye Aponyaye Roho ni Mwenye Busara**

**Mahali:** Nyumba ya Bibi Pili

**Waigaji Mchezo Huu:** Bibi Pili na Ruth

**Bibi Ruth:** U hali gani, Bibi Pili?

**Bibi Pili:** Salama salama, asante sana, nawe u hali gani?

**Bibi Ruth:** Mimi salama. Nimekuja kutoka kanisa la Kibatisti.

**Bibi Pili:** Ingia ukae. Nimefurahi sana kwamba umekuja. Nafikiri kwamba nalikuona dukani jana.

**Bibi Ruth:** Ndiyo, mwenye duka aliniambia kwamba ulihamia kijiji chetu.

**Bibi Pili:** Twapenda sana kijiji hiki. Watoto wamepata nafasi kusoma shuleni hapa.

**Bibi Ruth:** Unao watoto wangapi?

**Bibi Pili:** Ninao watoto wawili. Mmoja ana umri wa miaka minane na mwingine kumi.

**Bibi Pili:** Wameanza kuhudhuria Shule ya Jumapili?

**Bibi Pili:** La, hawajaanza, lakini wamepanga kuhudhuria Jumapili ijayo.

**Bibi Ruth:** Wewe ni mshiriki wa kanisa gani?

**Bibi Pili:** Sijajiunga na kanisa lo lote. Lakini nalihudhuria kwa kawaida nalipokuwa nyumbani.

**Bibi Ruth:** Wewe ni Mkristo, Bibi Pili?

**Bibi Pili:** Ndiyo...nafikiri mimi ni Mkristo. Nalihudhuria ibada ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Tabia yangu si mbaya. Mimi ni mwema kutosha kama washiriki wengine wa kanisa ambao ninawafahamu.

**Bibi Ruth:** Jambo hili laweza kuwa kweli, lakini wamjua Kristo kama Mwokozi wako? Je, umewahi kumpa moyo wako wote?

**Bibi Pili:** La, sijafanya hivyo.

**Bibi Ruth:** Je, unataka kufanya hivyo?

**Bibi Pili:** Ndiyo, nataka kufanya hivyo.

**Bibi Ruth:** Kristo ni wa maana sana kwangu hata nataka kukusaidia ili umjue pia. Je, unaweza kusoma Biblia yangu pamoja nami? Nitatafuta vifungu vinavyo-tuambia namna ya kuokolewa nawe usikilize ninaposoma. Kwanza ni lazima tufahamu kwamba sisi sote tumetenda dhambi kama vile kifungu hiki kinavyosema katika Warumi 3:23. (Soma kifungu hiki kutoka Biblia.) Hatuwezi kujiokoa sisi wenyewe, lakini Mungu ametupa njia kuokolewa. Yohana 3:16 husema hivi. (Soma kutoka Biblia yako.) Wokovu ni karama. Hatufanyi kazi ili tuupate wokovu. Bali unatoka kwake Mungu na kwa Yesu Kristo. Nasi tutaona kwamba hili limeandikwa jambo katika Waefeso 2:8,9. (Soma kutoka Biblia yako.) Je, twaweza kupata kipawa hicho cha wokovu? Turudi tena katika Warumi 10:10 na hapa twaona hivi. (Soma kutoka Biblia yako.)

Tutubu dhambi zetu na kuziacha dhambi hizo kabisa. Tumwamini Yesu na kumtegemea. Unafahamu hayo, sivyo?

**Bibi Pili:** Ndiyo nafahamu na tena naamini mambo hayo yote, lakini sikuzote nimekuwa na wasiwasi kama ningekuwa Mkristo singeweza kuendelea. Sitaki kuwa kama washiriki fulani wa kanisa.

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

**Bibi Ruth:** Ebu tusome Yohana 5:24. (Soma kutoka Biblia yako.) Unaweza kuona kwamba tunao uzima wa milele iwapo tunaamini. Utaamini yale inayoelezwa katika neno lake na kumtegemea Kristo?

**Bibi Pili:** Ndiyo, nitafanya hivyo, nitamwamini yeye.

**Bibi Ruth:** Hili ndilo jambo la kufanya nawe hutakosa kuwa na furaha. Kristo anatutazamia sisi kumkiri mbele ya watu. Yatupasa kumkiri kanisani halafu kubatizwa. Hii ni amri yake. Ubatizo ni mfano wa yale yaliyo-tendeka kwa roho yetu. Tunazikwa kutoka maisha yale ya zamani na kuinuliwa katika maisha mapya ndani yake! Na ubatizo ni ushuhuda wetu kwamba sisi ni watu wake. Kanisa letu lina darasa la wachunguzi wanaotaka kubatizwa. Ni katika darasa hili waweza kujifunza maana ya kuwa mshiriki wa kanisa na maana ya kuwa Mkristo. Baada ya kumaliza darasa hili, unaweza kubatizwa na kuwa mshiriki wa kanisa. Je, wataka kufanya hivyo?

**Bibi Pili:** Ndiyo, hayo ndiyo nitakayo kufanya.

**Bibi Ruth:** Ninayo furaha sana. Ebu, tuombe pamoja. (Wanawake wote wawili wasimame na kuinamisha vichwa vyao naye mwingine aimbe 'Nitwae Hivi Niliyyo' Tenzi za Rohoni, Namba 49.)

## MWISHO WA MCHEZO

### MAOMBI:

Waombee wanawake wale ambao majina yao yameandikwa katika orodha ile ya maombi.

## MPANGO WA KUMI

### USHIRIKA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI

Wimbo: Tangazeni Neno Lake  
Maombi

#### KIONGOZI:

Leo tutajifunza juu ya chama cha wanawake katika Makanisa ya Kibatisti ya Afrika Mashariki. Chama hiki kinaitwa "Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili."

Wimbo Wetu ni: "Nataka Nimjue Yesu."  
Na tuuimbe pamoja.

#### NATAKA NIMJUE YESU

Nataka nimjue Yesu,  
Na nizidi kumfahamu,  
Nijue pendo lake,  
Na Wokovu wake kamili.  
Zaidi, zaidi, nimfahamu Yesu,  
Nijue pendo lake,  
Na Wokovu wake kamili.

#### KIONGOZI:

Kifungu cha kutuongoza cha Ushirika wa Wanawake kinapatikana katika 1 Wakorintho 3:9. Hebu na tukisome pamoja: "Sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu."

Mungu amewapa watu ambao wameokolewa haki ya kufanya kazi pamoja katika kazi ya kuwavuta wengine kwake. Sisi wanawake tu wafanya kazi ndani ya shamba la Mungu ambalo ni ulimwengu.

**SEHEMU YA KWANZA:** Sababu za Kanisa Kuwa na Ushirika wa Wanawake

Wanawake ndani ya Biblia walifanya kazi ndani ya kanisa kwa njia nyingi. Wanawake wa siku hizi wanapaswa kufuata mfano wao.

Katika Ushirika huo wanawake hufundishwa njia za kuishi maisha ya Kikristo. Wanafundishwa juu ya utumishi na maombi.


Kazi ya kueneza Injili ni kazi ya kila Mkristo. Wanawake hujifunza jinsi ya kushuhudia wengine kati ya jamii yao. Pia hujifunza habari za kazi ya Kikristo katika nchi nyingine ili wafahamu mahitaji ya watu wale ya Injili.

Katika Ushirika wetu wanawake pia hujifunza kufundisha watoto wao na wasichana juu ya kanisa.

**SEHEMU YA PILI:** Alama Yetu

Hii ni picha ya alama yetu. Alama yetu ina umbo la kichwa maradufu cha samaki, alama ambayo ilitumiwa siku za kwanza za Ukristo. Alama hii ilitumiwa na Wakristo kwa sababu katika lugha ya Kiyunani herufi za kwanza za jina la 'Yesu Kristo, Mwanâ wa Mungu, Mwokozi' ziliandikwa neno 'samaki'.

Kando kando ya ncha za alama hiyo kumeandikwa: "Umoja wa Wanawake, Makanisa ya Wabatisti." Katikati pana picha ya Biblia iliyofunguliwa mahali palipoandikwa kifungu cha Ushirika wetu: I Wakorintho 3:9, "Wafanya kazi pamoja na Mungu".



Juu ya Biblia iliyofunguliwa kuna mwenge unaotoa nuru, ambao ni dalili ya Mwokozi, ambaye ni Nuru ya ulimwengu. Ramani ya ulimwengu inaonyesha ya kwamba hakuna mpaka wa Injili, na hakuna mpaka wa madaraka ya wafuasi wa Kristo.

#### SEHEMU YA TATU: Kusudi Letu

Kusudi letu ni kushiriki ujumbe ule wa wokovu; kudhihirisha maisha ya Kikristo nyumbani na katika jamii; kusoma Biblia; kuomba peke yetu na pamoja na jamaa zetu kutoa zaka na sadaka zetu; kuwatumikia wengine na kueneza injili katika Afrika ya Mashariki yote hata na dunia nzima.

#### SEHEMU YA NNE: Mikutano Yetu

Wanawake katika makanisa mengi ya Kibatisti hukutanika mara moja kila juma. Wao huchagua siku ambayo inafaa kwa wote. Katika mikutano yao wao huimba na kuomba na kujifunza. Hufanya mipango ya kazi watakayofanya ya kusaidia makanisa yao na kushuhudia wengine. Baada ya mipango ikimalizika wanawake wa baadhi ya makanisa huenda huko na huko kushuhudia. Katika makanisa mengine, hupenda kubaki nyuma baada ya mkutano kwa funzo ya kushona na kupika.

#### SEHEMU YA TANO: Vitabu Vyetu

Mipango ya mikutano yetu inapatikana katika kitabu kiitwacho 'IWE NURU'. Kila kitabu kina mipango ya miezi mitatu. Kama inawezekana, utahitaji nakala moja kwa kila mwanachama.

Kila kiongozi anahitaji nakala moja ya 'Kitabu cha Maelezo.' Anaweza kutumia kitabu hiki kwa miaka miwili au mitatu kama akiwa mwangalifu.

Kila Ushirika unahitaji nakala moja ya 'Kitabu cha Ripoti'. Kitabu hiki kinaweza kutumiwa kwa mwaka mmoja. Vitabu hivi

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

vyote vinaweza kuagizwa kutoka:

~~Baptist Publications House~~ Kenya Bap

P.O. Box 30370

NAIROBI, Kenya

Macha

an

Jan 1971

Itakuwa bora kuagiza vitabu hivyo sasa kama hujafanya hivyo. Utatumia mipango hii kwa vyama vipya kwa majuma mengine matatu tu.

Uwe na hakika ya kufanya mpango wa kulipia vitabu hivi.

### MAOMBI:

Mwombe Mungu akuongoze unapoanzisha Ushirika wa Wanawake katika kanisa lenu.

### KIONGOZI: Maswali ya Kuuliza

1. Chama cha Wanawake katika kanisa la Kibatisti kinaitwaje?
2. Wimbo wao ni upi?
3. Rudieni Kifungu cha Kutuongoza.
4. Kitabu cha mipango kinaitwaje?

## MPANGO WA KUMI NA MOJA

### SHABAHA ZETU

**Wimbo:** Nataka Nimjue Yesu (More about Jesus)

**Maandiko Matakatifu:** 2 Timotheo 2:15

**Maombi**

**Wimbo:** Nimekombolewa na Yesu (Redeemed, How I Love to Proclaim it)

**UTANGULIZI:** Tuna shabaha tano katika Ushirika wa Wanawake. Tutajifunza shabaha hizi leo. Tutajifunza vilevile yale mambo ambayo tutafanya ili tuweze kuzifikia shabaha hizo.

**SEHEMU YA KWANZA:** Kupata Ufahamu

Ni lazima tujue na kufahamu kabla ya kuweza kutenda. Ufahamu huo ndio hatua ya kwanza ya kumtumikia Kristo. Shabaha yetu ni:

*Tutajaribu kuwa na ufahamu wa watu wote na kuwahurumia wale ambao wamepotea bila Kristo. Tutajaribu pia kuwa na ufahamu wa kazi yetu kama wanawake Wakristo. Tutaendelea kufanya mambo haya kwa kujifunza Biblia na kwa mafunzo yetu katika 'Iwe Nuru' na vitabu vingine vya Kikristo.*

Tutakuwa na mpango kila juma kutoka 'Iwe Nuru'. Katika kila mkutano tutasoma Biblia. Tutawahimiza wanachama wetu wote kujifunza Biblia zao nyumbani mwao na katika Shule ya Jumapili.

Tutajaribu kuwavuta wanawake wote na kanisa letu wajiunge na Ushirika. Viongozi wetu watajifunza kazi yao ili waweze kuongoza wengine.

## MIPANGO YA USHIRIKA MPYA

### SEHEMU YA PILI: Kukua Katika Maisha ya Kiroho

Maombi na uenezaji wa Injili hayawezi kutengânishwa. Ni maombi na ushirika na Mungu ambavyo huleta watu wakamjua Mungu na kufanya kazi yake.

*Tutajaribu kutia nguvu maisha ya kiroho ya washiriki kwa kuwavuta kuomba na kusoma Biblia katika mikutano yetu, nyumbani, na katika maisha ya kila mmoja binafsi.*

Na tufanye mambo haya ili tufikirie shabaha yetu:

Na tuombe pamoja katika mikutano yetu yote. Na tuombe kabla ya kwenda kushuhudia nje. Kila mwanamke anapaswa kuomba nyumbani na pamoja na jamaa yake. Pia anapaswa kuomba peke yake kila siku. Tuhudhurie ibada zote za kanisa letu.

Tukumbuke nyakati zote maalum za sala. Siku ya Maombi ni Jumatatu ya kwanza ya mwezi wa Novemba. Juma la Maombi ni juma la kwanza la mwezi wa Machi.

### SEHEMU YA TATU: Kuwa Mashahidi Wakristo

*Tutajaribu kuwaongoza washiriki kuwa mashahidi Wakristo kwa ushuhuda wa Kristo kwa waliopotea na utumishi wa jamii inayoonyesha upendo wa Kristo. Tutajitahidi kutia nguvu maisha ya Kikristo nyumbani na kati ya jamii.*

Katika Ushirika wa Wanawake kazi ya kushuhudia na utumishi katika jina la Yesu Kristo unaitwa 'Utumishi wa Jamii'. Kazi hii imepangwa kwa kusudi la kuwavuta wengine kwa Kristo ambao hawajaokolewa na kufanya jamii zetu kuwa mahali ambapo watu wanaishi kama Kristo.

Kila chama kipange kazi ya kufanya kila mwezi. Kama kundi lenyewe likipendezwa kuanzisha zaidi ya mpango mmoja, litakuwa ni jambo bora sana. Kila mshiriki anahimizwa kutenda mengi kama

inavyoweze kana. Kuna matendo mengi ambayo kundi lenu linaweza kufanya kama kuwatembelea waliopotea na wagonjwa.

### SEHEMU YA NNE: Kushiriki Mali Yetu

*Tutajaribu kuendeleza Wakristo kushiriki kwa njia ya kufundisha uwakili. Tutawatia moyo washiriki kutoa fungu la kumi na kutoa sadaka maalum kupeleka neno la Mungu katika sehemu nyingine za nchi yetu au dunia.*

Uwakili ni kutoa wakati wetu, uweza wetu, na pesa zetu kwa Yesu. Kila mwanamke anapaswa kutafuta njia za kuwa wakili mwema kwa yote ambayo Mungu amempa.

Kila mshiriki apate kila alichio nacho kwa njia ya uaminifu. Anapaswa kutoa sehemu ya kumi ya mali yake kwa kanisa kwa ajili ya kazi ya Mungu. Atumie iliyobaki kwa njia inayompendeza Mungu.

Wanawake wanayo matoleo mawili ya kusaidia kuitangaza Injili. La kwanza ni mwezi wa Novemba wakati wa Siku ya Maombi, na lingine katika mwezi wa Machi wakati wa Juma la Maombi.

### SEHEMU YA TANO: Kufundisha Watoto na Vijana

*Tutajaribu kuwafundisha watoto wetu na wengine juu ya Mwokozi wetu. Tutajitahidi kuongoza watoto na vijana kufahamu habari ya Kristo katika vyama vinavyokutanika katika siku za juma katika makanisa yetu.*

Ili tuweze kufahamu hivyo tuwafundishe watoto wetu wenyewe juu ya Yesu. Tunaweza vilevile kuanzisha vyama katika makanisa yetu vya wavulana na wasichana: Vyama hivi vinaitwa 'Wajumbe wa Yesu'. Wasichana ni madaraka maalum ya wanawake. Kwa sababu wanawake wanapenda wavulana wapate mafundisho ya Kikristo, wahimise kanisa ili limchague mtu mwanamume kuongoza chama cha wavulana.

## **MIPANGO YA USHIRIKA MPYA**

**KIONGOZI:** Unaweza kujibu maswali haya?

1. Mipango yetu ya kila juma hupatikana katika kitabu gani?
2. Ni kitabu gani tunachohitaji kusoma kila siku?
3. Siku ya Maombi huwako lini?
4. Juma la Maombi huwa lini?
5. Ni nini 'Utumishi wa Jamii'?
6. Ni sehemu gani ya mali yetu Biblia inayotuambia tutoe kwa kazi ya Bwana?
7. Ni kazi ya nani kufundisha watoto wetu habari za Mwokozi?
8. Chama cha wasichana katika kanisa la Kibatisti kinaitwaje?

## **MAOMBI YA KUFUNGA**

## MPANGO WA KUMI NA MBILI

### VIONGOZI NA WASHIRIKI NA KAZI YAO

Wimbo

Maandiko

Wimbo

Maombi

**KIONGOZI:** Viongozi wa Ushirika wa Wanawake wachaguliwe kila mwaka. Ni jambo bora kama kuwachagua kila mwanzo wa mwaka. Kama mtu amefanya kazi nzuri, washiriki wanaweza kupenda kumchagua tena, lakini wanaweza kumchagua mtu mwingine wakipenda. Kabla ya kuwachagua viongozi, ombeni kwa maongozi ya Mungu.

Viongozi hawa ni lazima wawe Wakristo waaminifu ambao ni washiriki wa kanisa la Kibatisti. Ni lazima wawe wanawake ambao watafanya kazi na bidii na kujitahidi kujifunza kazi yao. Wawe wanawake wanaopenda watu wengine na wajitoe kuwashuhudia wengine juu ya Kristo.

**SEHEMU YA KWANZA:** Kazi ya Mwenye Kiti

1. Huongoza mikutano yote.
2. Husimamia shughuli zote za chama.
3. Hutafuta njia za kuwaandikisha wanawake wa Kibatisti wote.
4. Hufanya mipango ya utumishi wa jamii, naye huiongoza kundi katika kazi hii.
5. Huwasaidia viongozi kujifunza madaraka yao kwa njia ya kusoma Kitabu cha Maelezo au kuhudhuria mikutano ya jumuiya ndogo au mkutano wa Wanawake Wabatisti wa Tanzania au Kenya.
6. Hutayarisha ripoti ya mwaka, akisaidiwa na mwandishi, naye hutuma ripoti hiyo kwa Afisi ya Wanawake.

**SEHEMU YA PILI:** Kazi ya Mwenye Kiti wa Mipango

1. Hutayarisha mpango wa kila mkutano kutoka 'Iwe Nuru'. Hutoa sehemu mbeleni ili wale watakaosoma watajiweka tayari. Hutumia washiriki wengi mbalimbali kwa kutoa mpango. Hupanga njia tofauti za kutoa mpango.
2. Hufanya Mipango ya Maombi.
3. Hushika mahali pa Mwenye Kiti akiwa hayuko.

**SEHEMU YA TATU:** Kazi ya Mwandishi (au Karani)

1. Huweka orodha kamili ya majina ya washiriki wote.
2. Huweka 'Kitabu cha Ripoti' kwa njia nzuri. Huandika majina ya viongozi na washiriki. Huandika jumla ya waliohudhuria kila juma na jumla ya sadaka iliyotolewa. Huandika kila mwezi kazi ambayo kundi litafanya kwa Utumishi wa Jamii.
3. Huweka hesabu ya sadaka zote na kuonyesha vile pesa hizo zilivyotumika.
4. Hutoa ripoti mara kwa mara kuhusu ushirika na kuhusu pesa.
5. Humsaidia mwenye kiti kutayarisha ripoti ya mwaka ilioko ukurasa wa mwisho wa *Kitabu cha Ripoti*.
6. Hutuma sadaka maalum kwenye anwani zilizoonyeshwa kwenye mpango.
7. Huwapa Wanawake Wakristo moyo wa kuwa mawakili waaminifu.

**SEHEMU YA NNE:** Jinsi ya Kuwachagua Viongozi Wenu

Kwanza, ombeni mpewe uongozi wake Mungu. Halafu waulize wanawake kutaja majina mawili au matatu ya wanawake kwa ajili ya kazi ya Mwenye Kiti. Hapo kila mmoja atapiga kura kwa yule ambaye anafikiria kuwa kiongozi mwema.

Baada ya Mwenye Kiti kuchaguliwa, mchagueni Mwenye Kiti wa Mpango kwa njia hiyo. Halafu mchagueni Mwandishi.

Fanyeni mambo hayo sasa kabla ya kuumaliza Mpango.

**SEHEMU YA TANO: Kujifunza Kazi Yao**

Kama ikiwa unacho 'Kitabu cha Maelezo', mpe kila mwanamke aliyechaguliwa nakala ili kwamba aweze kuanza kujifunza kazi yake. Mpe kiongozi wa mpango nakala ya 'Iwe Nuru' ili aweze kupanga jinsi ya kuanza mpango wa kwanza. Umpe Mwandishi *Kitabu cha Ripoti* ili aanze kukitumia. Fanya mambo hayo hivi sasa ikiwa mna vitabu hivyo. Ikiwa hamna vitabu hivyo, agizeni sasa, au mwuulizeni mmisheni au mchungaji wenu kuwasaidieni.

**MAOMBI:** Mwombeni Mungu kuongoza wanawake ambao mmewachagua. Ombeni kwamba wanawake wote watakuwa washiriki waaminifu.

**JAMBO LA KUFANYA:** Juma lijalo mpango utakuwa juu ya Jumuiya. Itakuwa vizuri mkikaribisha kiongozi wa Jumuiya ya Wanawake kueleza habari za kazi yake.

## **MPANGO WA KUMI NA TATU**

### **WANAWAKE WABATISTI WAJIUNGA PAMOJA**

**Wimbo:** Mungu Roho Kiongozi

**Ibada Fupi:** 1 Wakorintho 3:9, "Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu."

Mungu ametupa sehemu katika kazi yake. Washiriki wa Kanisa la Kibatisti hufanya kazi pamoja. Makundi ya makanisa hufanya kazi pamoja pia.

Biblia hutueleza njia nyingi ambazo Wakristo na makanisa ya kwanza walivyokuwa wakifanya kazi pamoja na wale wa makanisa mengine. Wakristo wa Uyahudi walipopatwa na njaa, makanisa ya Makedonia waliwasaidia na sadaka ili wapate chakula. Wakristo walipohama kutoka mji mmoja kwenda mwingine, waliwatafuta Wakristo wale wengine kwa Ushirika. Nyaraka za Paulo katika Biblia yetu zilitumwa kutoka kanisa moja kwenda kwa watu wengine na kuwapelekea Neno la Mungu.

Kwa njia nyingi Makanisa ya Kibatisti siku hizi hujiunga pamoja ili yasaidiane. Huombeana na kujifunza mtu kutoka kwa mwenzake. Huwa na ushirika pamoja. Hujiunga pamoja katika kushuhudia na kuhubiri katika sehemu nyingine, Roho wa Mungu huwaongoza Wakristo wanapojaribu kufanya kazi pamoja.

**Wimbo:** Kazi Tufanye Sasa

**UTANGULIZI:** Leo tutajifunza jinsi Wanawake wa Kibatisti hujiunga pamoja ili waweze kufanya kazi iliyo bora kwa Bwana wao. Tunaona vile wanawake wa kikwetu hujiunga pamoja katika Jumuiya, katika taifa na mwishowe katika ulimwengu mzima.

**SEHEMU YA KWANZA: Jumuiya Ndogo**

Mara nyingi makanisa ya Kibatisti yaliyoko mijini au katika majimbo hutunga Jumuiya yenye wajumbe kutoka makanisa yote ya Kibatisti. Wanawake wa makanisa hushiriki katika Jumuiya, lakini wakati mwingine hupenda kuwa na Jumuiya wao wenyewe. Wanawake hupenda kukutana ili wajifunze pamoja, wasikie habari za kazi ya makundi yale mengine, na kuwa na ushirikiano. Wakati mwingine wao hufanya kazi pamoja kwa shughuli maalum. Jumuiya moja ya wanawake humlipia nauli mwanamke mmoja mwafrika ili ayatembelee makanisa na kuwasaidia wanawake walio wachanga katika imani ya Kikristo. Jumuiya za wanawake hukutana mara mbili au tatu katika mwaka mmoja. Huwachagua viongozi wao ambao huiongoza mikutano na kujaribu kuwasaidia viongozi makanisani.

**SEHEMU YA PILI: Jumuiya Kuu**

Pengine Wabatisti wa taifa fulani hujiunga pamoja na kuiunda Jumuiya Kuu ili makanisa yaweze kuendelea pamoja katika kueneza injili, kuwafundisha watu, na kuhudumu katika haja za watu. Katika Jumuiya Kuu, wanawake huwa na idara yao. Huwachagua viongozi wao ambao huwaongoza wanawake katika mikutano yao. Wanawake hushirikiana na Jumuiya Kuu katika mipango yake. Ushirika wa Wanawake Wabatisti wa Kenya Nzima huwapatia wanawake nafasi ya kujifunza na kushirikiana.

**SEHEMU YA TATU: Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Bara Afrika (Baptist Women's Union of Africa)**

Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Bara Afrika umeundwa na wajumbe kutoka makundi ya wanawake wa nchi za Afrika ambako kunayo kazi ya Kibatisti. Umoja huu hukutana kila miaka mitano. Ndio kiungo cha kutuunganisha sisi na wanawake Wabatisti katika Afrika na pande zote za dunia.

## **MIPANGO YA USHIRIKA MPYA**

**Makusudi ya Umoja huu ni:**

1. Kuendeleza ushirika mwema, kuwa na huruma kubwa, na kufahamu kamili kati ya Wanawake wa Kibatisti wa Afrika.
2. Kuwatia moyo wanawake kuungana pamoja kwa utumishi wa Kikristo.
3. Kuungana pamoja na wanawake wengine Wabatisti wa ulimwengu katika Siku ya Maombi.

**SEHEMU YA NNE:** Mwingano wa Wabatisti wa Ulimwengu (Baptist World Alliance)

Mwingano wa Wabatisti wa Ulimwengu umefanywa na makundi ya Wabatisti kutoka pande zote za ulimwengu. Chama hiki kinakutana baada ya kila miaka mitano.

Mojawapo ya sehemu za Mwingano wa Wabatisti wa Ulimwengu ni Idara ya Wanawake. Kuna Umoja wa Wanawake Wabatisti katika kila bara kuu, yaani tano. Tunahusika na Idara ya Wanawake kwa njia ya uanachama wetu katika Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Bara Afrika.

Siku ya Maombi ya Wanawake Wabatisti wa Ulimwengu inatayarishwa na Idara ya Wanawake kila Jumatatu ya Kwanza ya mwezi wa Novemba. Tunaungana na wanawake wa mataifa yote siku ile tukiomba pamoja.